SEKTA YA BIASHARA NA VIWANDA KATIKA MKOA WA KILIMANJARO

A. VIWANDA

Mkoa wa Kilimanjaro kihistoria ni Mkoa ambao ulikuwa na viwanda vingi ambavyo vilichangia sana kuinua pato la wananchi wa mkoa huu na pato la Taifa kwa ujumla. Viwanda hivyo kwa sasa vingi vimefungwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa malighafi, ushindani wa bidhaa toka nje ya nchi, bidhaa zinazoingia Mkoani toka nchi jirani kwa njia zisizo rasmi na ukosefu wa teknolojia ya kisasa inayohimili ushindani wa soko, na pia baadhi ya wawekezaji walionunua viwanda vilivyokuwa vya serikali kutokuwa na nia thabiti ya kuviendeleza. Moja ya viwanda hivyo ni pamoja na Kiwanda cha *Kilimanjaro Mashine Tools Manufacturers Ltd* kilichopo Hai; Kiwanda cha madawa ya kilimo cha *Twiga Chemicals Ltd* kilichopo Moshi; Kiwanda cha bidhaa za mbao (*Kiliwood Products Ltd*) kilichopo Moshi; Kiwanda cha viberiti (*Kibo Match Ltd*) kilichopo Moshi; Kiwanda cha karatasi (*Kibo Paper Ltd)* kilichopo Moshi; Kiwanda cha magunia (*Tanzania Packaging Manufacturers (1998) Ltd)* kilichopo Moshina Kiwanda cha kukoboa mpunga cha *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd* kilichopo Chekereni – Moshi.

Mkoa una viwanda vikubwa tisa (9) vinavyofanya kazi vizuri ambapo uwepo wa viwanda hivi pamoja na viwanda vingine vidogo vidogo katika Mkoa wa Kilimanjaro vimesaidia sana kutoa ajira kwa wananchi wetu, kuinua pato la Mkoa, Taifa kwa ujumla. Viwanda hivyo ni kiwanda cha sukari cha TPC kilichopo Moshi; kiwanda cha bia cha *Serengeti Breweries Ltd* Kilichopo Moshi; Kiwanda cha *spirit* cha *Kilimanjaro Biochem Ltd* kilichopo Mwanga; Kiwanda cha bidhaa za mbao (*Imara wood Products Ltd*); Kiwanda cha ngozi (*Moshi Leather Industries Ltd*); Kiwanda cha ngozi cha Himo (*Himo Tanneries Ltd*); Kiwanda cha Saruji (*Moshi Cement Ltd*) kilichopo Rombo; Kiwanda cha vinywaji baridi cha *Bonite Bottlers Ltd* kilichopo Moshi na Kiwanda cha *Bella view Fresh Fruits Company Limited* kilichopo wilaya ya Rombo.

Ufufuaji na uanzishaji wa viwanda vipya

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba 2017 hadi Machi 2020, mkoa umefanikiwa kuanzisha viwanda vipya 113 ambavyo vimeweza kuzalisha ajira 912 kwa mtaji wa jumla ya Tsh. 3,813,800,000. Kati viwanda 113 vilivyoanzishwa hadi sasa, viwanda 80 ni **vidogo sana** (*Micro*), viwanda 26 ni **vidogo** (*small)*, viwanda 4 ni vya **kati** (*medium*) na viwanda 3 ni **vikubwa** (*large*). Mchanganuo wa viwanda vilivyoanzishwa kwa kila halmashauri ni kama inavyoonekana kwenye jedwali:

Na	**Halmashauri**	Idadi ya viwanda vya zamani kabla ya Novemba 2017	Lengo (*target*) kwa kila halmashauri	**Jumla viwanda vipya** vilivyoanzishwa **Des 2017 - Machi 2020**	Asilimia ya utekelezaji wa lengo (%)	Ajira zilizozalishwa	Mtaji uliotumika (Tshs. Milioni)
1	Siha	70	15	**17**	**113.3**	396	877.8
2	Hai	14	14	**10**	**71.4**	54	263
3	Moshi MC	71	15	**24**	**160.0**	155	380
4	Moshi DC	11	14	**15**	**107.1**	170	618
5	Rombo	76	14	**14**	**100.0**	51	621
6	Mwanga	36	14	**17**	**121.4**	45	733.5
7	Same	9	14	**16**	**114.3**	41	314.5
	Jumla	**287**	**100**	**113**	**113**	**912**	**3,813.8**

Ufufuaji wa viwanda visivyofanya kazi

Kipaumbele cha mkoa ni kufufua viwanda vilivyopo ambavyo kwa sasa havifanyi kazi ili vifanye kazi na kutoa ajira kwa wananchi ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa tayari umeanza uhamasishaji wa wadau mbalimbali ikiwemo mifuko ya hifadhi ya jamii kujitokeza ili kuja kufufua viwanda hivyo. Juhudi hizo tayari zimeanza kuzaa matunda na baadhi ya wadau wameonesha nia ya kuja kusaidia kuvifufua na kuviendeleza kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:

Na	Kiwanda	Hali ya Kiwanda	Juhudi zilizofanyika
1.	Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools	• Kiwanda kinamilikiwa na shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), • Kiwanda hiki kwa sasa kinatengeneza mikokoteni (tela) za kuvutwa kwa trekta kwa ajili ya kubebea mazao shambani. Hadi Desemba 2019 jumla ya matela 40 yalikuwa yameshatengenezwa.	• Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) lina mpango wa kufufua kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools katika awamu tatu kwa gharama ya Tsh. 10.295 Bilion. Awamu ya kwanza itahusisha kujenga tanuru la kufua vyuma na ukarabati wa power house, awamu ya pili ni uzalishaji wa bidhaa mpya kwa kutumia mashine za kufua vyuma na awamu ya tatu ni ujenzi wa kiwanda kikubwa. • Bodi ya Ex-GEPF ilikuwa tayari imeidhinisha mkopo wa shilingi bilioni 1.665 kwa riba ya 14.5% kwa ajili ya kujenga tanuru dogo pamoja na kurekebisha mfumo wa umeme kiwandani, • Kinachosubiriwa sasa ni NDC kupata vibali muhimu kutoka Wizara ya Fedha.
2.	Kiwanda cha Kilimanjaro Industrial Development Trust (KIDT) tawi la Same.	• Kiwanda hiki kipo chini ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa, • Kiwanda hiki kinazalisha bidhaa mbalimbali za udongo kama vile vyombo vya mezani na vikombe vya umeme, (insulators) • Uzalishaji wa kiwanda ni mdogo sana kutokana teknolojia duni pamoja na kuchoka kwa tanuru.	Uongozi kwa sasa unatafuta wawekezaji ili waingie nao ubia.
3.	Kiwanda cha Tangawizi cha Mamba myamba Ginger Growers Cooperative Society	• Kiwanda kinamilikiwa na Ushirika wa Wazalishaji wa Tangawizi kata ya Mamba Myamba, • Kiwanda kinasindika Tangawizi, • Kiwanda hakifanyi kazi kwa ufanisi kutokana na teknolojia duni yenye uwezo mdogo na iliyopitwa na wakati.	• Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa LAPF (PSSSF sasa) ulikubali kuingia ubia na wamiliki wa kiwanda kwa njia ya hisa ili waweze kukiboresha kwa kufunga mashine mpya za kisasa za kuchakata tangawizi. Mgawanyo wa hisa ni PSSSF 60% na Ushirika wa Tangawizi 40%. • Ushirika wa wakulima wa Tangawizi tayari wameunda kampuni itakayosimamia utekelezaji na uendeshaji wa kiwanda inayojulikana kama ***Mamba Ginger Growers Company Ltd*** • Kampuni imesainiana Mkataba wa makubaliano (MoU) na PSSSF - (LAPF) ambao wamekubali kutoa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kununua mashine mpya. • Mashine zimeshaagizwa Nchini China hivyo

			mwezi Aprili zinategemewa kufika na kufungwa.
4.	Kiwanda cha Viatu Karanga (Cha zamani)	• Kiwanda hiki ni cha zamani kinafanya kazi, • uzalishaji ni jozi za viatu 146 tu kwa siku	PPF kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza tayari wameunda kampuni inayojulikana kama ***Karanga Leather Industries Company Ltd*** ambayo itasimamia utekelezaji na uendeshaji wa mradi, • Mashine mpya zilizofungwa zinaongeza uzalishaji wa viatu kutoka jozi 146 kwa siku hadi jozi 450 - 600 kwa siku.
5.	Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Karanga (Kipya)	• Kiwanda hiki kipo kwenye ujenzi kwa sasa	• Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSSSF (PPF) waliingia ubia na Jeshi la Magereza kwa ajili ya kujenga kiwanda kipya na cha kisasa chenye thamani ya shilingi bilioni 55.44 kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za ngozi; • Kampuni ya ***Karanga Leather Industries Company Ltd*** ndiyo yenye jukumu la kusimamia ujenzi na uendeshaji wa kiwanda hiki; • Mradi huu upo kwenye hatua ya mwisho ya ujenzi na ukikamilika unatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja kwa watanzania zaidi ya 1200.
6.	Kiwanda cha Magunia	• Kiwanda kinamilikiwa na Mohamed Enterprises Ltd, • Kiwanda hiki hakifanyi kazi tangu kimenunuliwa mwaka 2006	• Mwekezaji huyu ameshakarabati jengo kwa kupaka rangi ila hadi sasa bado ajaweka mashine kwa ajili ya uzalishaji wa magunia. • Serikali ya Mkoa ilitembelea eneo ilo pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara mwezi Machi 2020 na kumtaka mwekezaji atekeleze maagizo ya kufufua kiwanda hicho na kama hataweza harudishe kiwanda Serikalini.
7.	Kiwanda cha Madawa ya Kilimo cha Twiga Chemical Manufacturers	• Kiwanda hiki kinamilikiwa na kampuni ya Twiga Chemical Industries Ltd, • Kiwanda hakifanyi kazi	• Kiwanda hiki bado ni kipya kabisa lakini hakifanyi kazi yenye tija kwani Mwekezaji ameonekana hana nia ya dhati ya kuendeleza kiwanda hiki. • Kutokana na mwekezaji wa kiwanda hiki kutokuwa na nia thabiti ya kuendeleza kiwanda hiki, Serikali kupitia Ofisi ya msajili wa hazina imerudisha kiwanda hiki Serikalini tangu tarehe 18/10/2018 na baadae atatafutwa mwekezaji mwingine ili aendeleze shughuli za uzalishaji kiwandani hapo.
8.	Kiwanda cha bidhaa za mbao (Kiliwood Products)	• Kiwanda kinamilikiwa na Hans Industries • Kiwanda hakifanyi kazi	• Kutokana na mwekezaji wa kiwanda hiki kutokuwa na nia thabiti ya kuendeleza kiwanda hiki, Serikali kupitia Ofisi ya msajili wa hazina imerudisha kiwanda hiki Serikalini na baadae atatafutwa mwekezaji mwingine ili aendeleze shughuli za uzalishaji kiwandani hapo

9.	Kiwanda cha kukoboa mpunga cha Kilimanjaro Paddy Hulling Company Ltd.	• Kiwanda hiki hakifanyi kazi tangu Septemba 2014.	• Kiwanda cha kukoboa mpunga kilikodishiwa kwa chama kikuu cha Ushirika (KNCU) na baada ya kushindwa kukiendesha, mkoa ulimshauri msajili wa Hazina kukirudisha serikalini ili atafutwe mwekezaji mwingine anayeweza kukiendesha. Tayari Msajili wa Hazina amerejesha kiwanda hiki serikali tangu tarehe 18/10/2018

Changamoto za Mkoa katika uwekezaji kwenye viwanda

- Maeneo mengi ya uwekezaji kutopimwa, kwa kuanzia zinahitajika fedha za fidia na za upimaji, na kuweka miundombinu muhimu kama vile maji, umeme na barabara kabla ya kutangazwa kwa wawekezaji;
- Uhaba wa ardhi ya kufanyia uwekezaji;
- Ugumu na urasimu katika upatikanaji wa mitaji umekuwa ukikwamisha wawekezaji wengi kuwekeza katika viwanda.

Mikakati ya mkoa ya utekelezaji wa ujenzi wa viwanda

- Kuendelea kusambaza mwongozo wa uwekezaji ulioandaliwa na mkoa kwa wadau wa nje na ndani ya mkoa kutoa fursa kwa wadau wengi kujua fursa za uwekezaji zilizopo mkoani;
- Mkoa umeelekeza Halmashauri kuendelea kutenga maeneo ya uwekezaji na kuweka utaratibu wa kupima maeneo hayo. Mfano maeneo yaliyotengwa hadi sasa ni Same (ekari 4000 eneo la Makanya ekari 150 eneo la stesheni), Mwanga (ekari 1800 maeneo ya mgagao, kileo na mwanga mjini kwa ajili ya viwanda na biashara), Rombo (ekari 254.31 eneo la Holili), Moshi DC (ekari 3,080 soko estate, ekari 140 makuyuni, na ekari 9.6 eneo la njia panda); Moshi MC (ekari 37.5 maeneo ya Soweto, majengo, kaloleni, shia na korongoni); Hai DC (ekari 714 maeneo ya sanya station, Weruweru, kimashuku, KIA, Hai mjini na eneo la Mashine Tools); Siha DC (ekari 7,267 zimetengwa maeneo ya Ngarenairobi).
- Mkoa umepanga kufanya Kongamano la Uwekezaji la Mkoa kwa ajili ya kuutangaza Mkoa pamoja na fursa za uwekezaji kwa kushirikiana na kampuni ya magazeti ya serikali *Tanzania Standard News Papers* (TSN). Kupitia tamasha hilo,

fursa mbalimbali za uwekezaji kupitia kilimo, viwanda, utalii, biashara na nyinginezo katika mkoa zitatangazwa na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kutoka ndani na nje watapata fursa;

B. UANZISHAJI WA MASOKO YA MADINI

Mkoa wa Kilimanjaro unayo hazina kubwa ya madini ambayo yameshagundulika na kuanza kuchimbwa, na pia mengine yamegundulika lakini changamoto imeonekana yako kwenye hifadhi za misitu na Hifadhi ya wanyamapori ya Mkomazi. Baadhi ya madini yanayopatikana hapa Mkoani ni pamoja na bauxite, gypsum, magnesite, feldspar, Talc, vermiculite, graphite na mica, Garnet, ruby/Zoisite, na Zircon, dhahabu, chuma, shaba, Pozollana, Rhodolite, sulphur na madini ya chokaa.

Sekta ya madini hapa Mkoani Kilimanjaro inachangia pato la Taifa kutokana na malipo ya mrabaha kwa serikali pamoja na ada ya ukaguzi. Katika kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2019 sekta hii imeweza kuchangia mapato ya serikali hapa mkoani kama ifuatavyo: mwaka 2014 sekta ilichangia jumla ya shilingi **417,491,923.50,** mwaka 2015shilingi **1,100,512,059.19,** mwaka 2016 shilingi **885,067,402.68,** mwaka 2017 shilingi **725,853,858.11,** mwaka 2018 shilingi **773,366,298.41** na mwaka 2019 shilingi **936,510,303.**

Mkoa kwa kushirikiana na Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Kilimanjaro; tumeanzisha soko la madini katika Wilaya ya Same na linaendelea kufanya kazi. Mkoa tunaendelea na taratibu za kuanzisha soko lingine la madini katika Manispaa ya Moshi na tayari jengo limepatikana linafanyiwa ukarabati.